## Hoja za mjadala wa kijumla kuhusu kuisha kwa mafao ya chakula cha dharura cha SNAP ya COVID-19 (Mgao wa Dharura wa SNAP)

***Ujumbe kwa washirika:*** *Hoja hizi za mjadala zinatolewa kama mwongozo wa mjadala na hazipaswi kusambazwa. Mjadala huu unapaswa kugeuzwa ili ushughulikie mahitaji maalum ya mtu binafsi na maswali. Nyenzo za msaada zimeorodheshwa hapo chini.*

- Tangu Aprili 2020, watu wengi katika Oregon wanaopokea SNAP pia wamepokea mafao ya chakula cha dharura kila mwezi kwenye kadi yao ya EBT (Oregon Trail). Mafao haya yalibuniwa na serikali kuu ili kusaidia katika dharura ya afya umma ya COVID-19.
    - Mafao ya chakula cha dharura ni kiasi cha fedha za ziada zinazoongezwa kwenye kadi za EBT katika siku ya 11 au 12 ya mwezi.
- **Februari utakuwa ni mwezi wa mwisho wa kuruhusiwa kwa mafao ya chakula cha dharura. Watu wanaopokea SNAP wataendelea kupata mafao yao ya SNAP mwezi wa Machi 2023 na kila mwezi baada ya Machi.**
    - Mafao ya SNAP ni kiasi cha fedha ambacho watu wanapata kwenye kadi zao kati ya siku ya 1 na siku ya 9 ya kila mwezi.
- Kwa miaka miwili, ODHS imekuwa ikitoa mafao ya chakula cha dharura kwa mamia ya familia zinazopokea SNAP.
    - Mafao haya yameongeza pakubwa uwezo wa watu kupata chakula chenye afya bora kwao binafsi na familia zao.
    - Bila mafao haya ya chakula dharura baadhi ya watu wa Oregon wanaweza kukumbwa na hali ngumu na kuhangaika kukidhi mahitaji yao ya msingi.
- Watu wanaweza kuangalia akaunti yao ya ONE au akaunti ya EBT Edge ili kuona kiwango kamili cha mafao yao ya chakula cha SNAP bila mafao ya chakula dharura:
    - Kwenye dashbodi ya ukurasa wa akaunti ya ONE – kiwango cha kawaida cha fedha kwenye SNAP kitaorodheshwa chini ya "Fedha za Mafao ya Mwezi"
    - Katika shughuli za akaunti yao ya EBT Edge – kiwango cha kawaida cha fedha za SNAP kitakuwa ndicho kiwango kinachoongezwa kwenye kadi yako kati ya siku ya kwanza na ya 9 kila mwezi.
- Watu binafsi na familia ambazo zimeathirika zinapaswa kuwasiliana na washirika wa jimbo na mitaa haraka iwezekanavyo ili wafanye mpango wa kukidhi mahitaji yao ya chakula baada ya kupokea mafao chakula cha dharura cha mwezi wao wa mwisho. Nyenzo zinajumuisha:
    - Taarifa ya 211: Piga simu 2-1-1 au tembelea [www.211info.org/](http://www.211info.org/)

    - Nyenzo za Muunganisho wa Oregon kwa Wazee na Walemavu (Aging and Disability Resource Connection of Oregon, ADRC): Piga simu 1-855-673-2372 au tembelea www.adrcoforegon.org/
    - Mabenki ya chakula ya Oregon www.oregonfoodfinder.org/
    - Benki au bohari la chakula katika eneo lako
    - Mashirika ya Huduma za Kijamii katika eneo lako: www.caporegon.org/
    - Nyenzo zingine zozote za kieneo ambazo ungeweza haswa kuwapendekezea watu walio na matatizo ya kugharamia chakula cha kutosha.
- Familia pia zinaweza kunufaika kutokana na mipango hii ya jimbo na serikali kuu ili kulipia gharama zao zingine:
    - **Mpango wa Msaada wa Nishati ya Kinyumbani kwa Walio na Mapato ya Chini (Low Income Home Energy Assistance Program, LIHEAP)** unasaidia katika kuwaweka watu salama na wenye afya kupitia kwa mipango inayosaidia watu binafsi na familia zao kumudu gharama za nishati. Tembelea EnergyHelp.us au piga simu 1-866-674-6327 kwa taarifa kuhusu jinsi ya kutuma ombi la msaada wa nishati.
    - **Msaada wa ziada wa bili za matumizi** (Additional utility bill assistance unatolewa na Oregon Housing and Community Services, OHCS) kupitia kwa mashirika ya kieneo. Unaweza kutuma ombi kwa shirika la eneo lako kwa tovuti yao: https://www.oregon.gov/ohcs/energy-weatherization/Pages/utility-bill-payment-assistance.aspx.
    - **Mpango wa Muunganisho Nafuu** unatoa angalau $30 za mapunguzo kwa huduma za intaneti kwa familia zinazo hitimu. Ikiwa unapokea mafao kutoka ODHS, unaweza kuhitimu moja kwa moja. Ili kuangalia ustahiki wako au kuwasilisha ombi lisilo la hatari bila malipo, tembelea GetInternet.gov au piga simu 1-877-384-2575.
    - **Msaada wa ukodeshaji nyumba na makazi** unatolewa kupitia OHCS. Tembelea Tovuti ya OHCS kwa https://www.oregon.gov/ohcs/housing-assistance/Pages/housing-assistance.aspx.